

Ungano la vijana (Youthlink) husaidia vijana wa umri wa miaka 13-24, wanaokuwa na matatizo ya hali njema zao za kihisia na kijamii. Tunatoa huduma ya ushauri nasaha wa bure na wa siri na wafanyakazi wenye uzoefu mkubwa, urafiki, kuthamini mawazo ya wengine na kukubali watu. Tunaweza kukupatia ukalimani wa bure kukusaidia na mawasiliano na ikihitajika, tunaweza kufikia kwako.

Tunaheshima utamaduni, jinsia na maumbile mbalimbali na ulemavu. Baadhi ya mifano ya maswala ya afya ya kihisia na kijamii ambayo tunayoweza kukusaidia yakiwemo: mfadhaiko, huzuni na hasara, mawazo ya kujiumiza, mkazo, kutumia pombe na dawa ya kulevya, hasira na shari, kujiamini na uhusiano wa matatizo.

Kwa kuongezea, tunaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma nyingine saidizi. Tunaweza kukusaidia kuwa na mbinu za kushauriana na kuwasiliana na jamaa zako na watu wengine, na tunaweza kutetea kwa ajili yako.

Tupo wazi Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2.30 asubuhi mpaka saa 10.30 alasiri (yaani, 9.00am – 5.00 pm). Tupo 223 Barabara ya James, Eneo la Northbridge, Australia Magharibi.

Ukitaka kuongea nasi umpigie simu Ofisa wa Kiingizio 1300 362 569. Pia unaweza kumwomba mtu mzima ambaye unamwamini kutupigia simu kwa ajili yako. Utujulishe ukitaka tupange mkalimani wa simu wa lugha yako.